TANGAZO LA SERIKALI NA.173 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA CHAMBO YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Chambo ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 223 yenye majira - nukta 457680MS, 9537109KZ; baada ya hapa mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KZ61°14’03”MS kwa umbali wa kilomita 6.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 212 yenye majira - nukta 463083MS, 9540050KZ; baada ya hapo

mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS16°33’05”MS kwa umbali wa kilomita 6.51 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 221 yenye majira - nukta 464904MS, 9533869KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS66°35’05”MG kwa umbali wa kilomita 4.99 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 222 yenye majira – nukta 460316MS, 9531878KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ26°39’10”MG kwa umbali wa kilomita 5.85 hadi ulipoanzia.”

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*